



MTWA MKWAWA MUSEUM MKWAVINYIKA – KALENGA, IRINGA

Kiswahili





Introduction:

Makumbusho Kumbukizi ya "Mtwā" Mkwawa ni kituo kilichohifadhi historia ya wabartu kabila la Wahehe. Ingawa asili ya ukoo wa Mwamuyinga ulitokana na mtu mmoja muwindaji wa kabila la Wakamba. Kabila hili la wahehe lilikuwa shupavu lenye kupigana vita na kushinda mwishoni mwa karne ya 18 na 19.

Mkwawa "Mtwā" yaani Chifu aliyekuwa shupavu na aliyewashinda wajerumani katika vita huko Lugalotarehe 17 Agosti 1891 kwa kuwauwa maaskari 300 na bwana mkubwa wao Emily Von Zelewisky. Vita vya pili kati ya Wahehe na Wajerumani 28 Oktoba 1894 - 98 ambapo Mkwawa alijiua kwa kwa kujipiga risasi maeneo ya Mlambalasi. Wajerumani



walikata kichwa cha Mkwawa na kukipeleka Ujerumani Makumbusho mjini Bremen. Fuvu lakichwa cha Mkwawa lilirudishwa Tanzania tarehe 19 Juni 1954 na sasa limehifadhiwa makumbusho kijiji cha Kalenga. Jina la Mkwawa limetokana na neno Mukwavinyika likimaanisha mtu aliyeshinda tawala nyingi au mtekaji wa nyika.

Park History

Kalenga ilitokana na neno "Kwilenga/Lulenga" yaani panapopatikana maji. Hapo palitengenezwa ngome ya mawe iliyopata umaarufu wa jina la "Lipuli" linatokana na neno "Tulipwe" wakimaanisha tumemaliza ngwe yetu. Kuta za ngome zilikuwa na urefu wa futi 12 upana futi 03 na ukubwa wa ngome ulikuwa ni Km 16. Ngome ya Lipuli ilitengenezwa kwa mawe wa miaka minne (04) kuanzia 1887 - 1891. Ngome hii ilitengenezwa kwa kusudi ya kukabiliana na Wajerumani baada ya kuwasikia wapo Pwani wakipambana na kuchukua himaya za huko. Wahehe waliamini sana ngome yao na walidhani hakuna kitakachoidondosha lab da kiwe kilichotoka mawinguni.



Getting there:

Kunafikika kwa njia ya miguu au vyombo vya moto gari, pikipiki, miguu. Eneo hili linapatikana nyanda za juu Kusini mkoa wa Iringa, Iringa imepakana na mkoa wa Dodoma, Morogoro, Njombe na Mbeya. Mkoa wa Iringa una Wilaya nne, Iringa Vijijini, Kilolo, Mufindi na Wilaya ya Iringa mjini ilipo makumbusho ya "Mtwi Mkwawa". Tarafa ya Kalenga kijiji cha Kalenga, toka Iringa mjini mzunguko wa Samora ni Km 10 upande wa magharibi barabara iendayo pori la hifadhi ya wanyamapori Ruaha.

Tourism Activities

Kituo cha Makumbusho ya "Mtwā" Mkwawa kinatoa shughuli zifuatazo kiutalii:-

- (i) Utalii wa utamaduni
- (ii) Maelekezo ya kihistoria
- (iii) Kutembelea Makumbusho

Attraction

- (i) Makumbusho -Iliyo hifadhi fuu la "Mtwā" Mkwawa na vifaa alivyotumia wakati wa uhai wake.
- (ii) Ngome ya Lipuli ambayo ni mabaki ya kuta
- (iii) Mnara wa Lugalo -Ambapo maaskari ho dari wa kijerumani 300 na bwana mkubwa wao walizikwa kwa pamoja.
- (iv) Mlambalasi - Kaburi la kiwiliwili cha "Mtwā" Mkwawa na ulipo mnara wa kumbukumbu baada ya miaka 100 ya kifo cha mtwa Mkwawa.
- (v) Kikongoma - Daraja la Mungu pia ni mahali alipojiua mama yake Mkwawa.





Rules and Regulations:

- Usiguse wala kushika kitu ndani ya Makumbusho
- Usipige picha fuvu
- Vua viatu kabla ya kuingia makumbusho
- Usiingie makumbusho na chakula, maji au mabegi makubwa
- Tunza mazingira ya kituo

Tariffs:

Conservation Fee	East Africa (TShs)	Non Resident (USD)	Expatriate (USD)
i. Of or above age of 16 years	2,000	10	5
ii. Between the age of 5 and 15 years	1,000	5	2.5
iii. Children below the age of 5 years	Free	Free	Free

All tariffs are VAT (18%) exclusive

Payments are done by VISA, Master credit cards of any bank, Mpesa, Tigo Pesa, Airtel Money ect.

Working Days


Monday-Friday

Saturday, Sunday and
Public Holidays

Working Hours

08:00 A.M. - 05:30 P.M.

08:00 A.M. - 05:00 P.M



Ngome ya Mtwawa Mkwawa Mkwavinyika Lipuli Kalenga

For more information:

Mtwawa Mkwawa Museum

P. O. Box 369

Kalenga, Iringa - Tanzania

Tel: +255 764 330 913 / 652 509 857

Email: mkwawa@tanzaniaparks.go.tz

Instagram: [mkwawa_museum](https://www.instagram.com/mkwawa_museum)